


Kwanini Viboko Hawana Nywele



- ✎ Basilio Gimo, David Ker
- ⌚ Carol Liddiment
- 💬 Matteo E. Mwita
- 💬 Kiswahili
- 🔊 Level 2




Siku moja, Sungura alikuwa
akitembea pembeni ya mto.



Kiboko alikuwepo pia, akitembea
huku akila majani mazuri ya kijani.



Kiboko hakumwona Sungura na kwa bahati mbaya akaukanyaga mguu wa Sungura. Sungura akaanza kumpigia Kiboko kelele. “We Kiboko huoni kama umeukanyaga mguu wangu?”



Kiboko akamwomba Sungura msamaha, "Samahani, sikukuona, tafadhali nisamehe!" Lakini Sungura hakukubali na akaendelea kumbwatukia Kiboko, "Umfanya makusudi! Kuna siku utakiona, na nitakulipizia!"

Sungura alienda kutafuta moto na akamwambia, “Nenda, ukamchome Kiboko akitoka majini kuja kula majani. Alinikanyaga!” Moto ukajibu, “Hakuna tatizo, rafiki yangu Sungura, nitafanya ulichoniomba kufanya.”





Baadaye, Kiboko alikuwa akila majani mbali na mto, aliposhtuka moto umelipuka. Miale ya moto ikaanza kuzichoma nywele za Kiboko.



Kiboko akaanza kulia na kukimbilia
kwenye maji. Nywele zake zote
zilikuwa zimeungua na moto.
Kiboko aliendelea kulia, "Nywele
zangu zimeungua na moto!
Nywele zangu zote zimeisha!
Nywele zangu nzuri!"

Sungura alikuwa na furaha kwa
kuwa nywele za Kiboko ziliungua.
Hadi leo kwa kuogopa moto,
Kiboko hawezি kwenda mbali na
maji.





Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Kwanini Viboko Hawana Nywele

Written by: Basilio Gimo, David Ker

Illustrated by: Carol Liddiment

Translated by: Matteo E. Mwita

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).